

TANGAZO LA SERIKALI NA. 428 la tarehe 31/5/2024

SHERIA YA FEDHA ZA KIGENI
(SURA YA 271)

—————
KANUNI
—————

(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 5(a) na 7)

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA MADUKA YA KUBADILISHA FEDHA ZA
KIGENI ZA MWAKA 2024

Jina
TS Na.
729 la 2023

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni za mwaka 2024 na zitasomwa kwa pamoja na Kanuni za Maduka ya Kubadilisha Fedha za Kigeni za mwaka 2023 ambazo katika Kanuni hizi zitajulikana kama “Kanuni kuu”.

Marekebisho ya
kanuni ya 3

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza katika mtiririko sahihi wa kialfabeti tafsiri ifuatayo:
Sura ya “Mkurugenzi” ina maana sawa na ile
212 iliyotafsiriwa kwenye Sheria ya
Makampuni.”

Marekebisho ya
kanuni ya 5

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5(1) kwa kufuta maneno “isipokua kama,” na kuweka badala yake neno “iwapo”.

Marekebisho ya
kanuni ya 7

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 7(1) kuingiza maneno “moja kati ya” katikati ya maneno “biashara” na “maneno”.

Marekebisho ya
kanuni ya 40

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya
40(1) kwa kufuta aya ya (b) na kuandika upya kama
ifuatavyo:

“(b) kutoza faini ya kiwango kisichozidi,
Dola za Marekani elfu tatu kwa
shilingi za Tanzania.”

Dodoma,
21 Mei, 2024

EMMANUEL M. TUTUBA
Gavana